

Unaelekea Kwenye Ushindi Au Kushindwa?

Kwa kweli, watu walio wengi hutaka kusimama mwishoni mwa maisha yao na kudai ushindi. Tatizo ni kwamba, watu wengi leo hawajui ushindi wa kweli ukoje. Wengine hudai kuwa ushindi uko katika idadi ya shahada walizotunukiwa au kiasi cha fedha walichojiwekea akiba, au kiwango cha umaarufu walioupata hapa duniani. Mshairi kafiri William Henley aliandika, “Mimi ndiye bosi wa hatima yangu; Mimi ni mkuu wa nafsi yangu.”

Walakini, kwa namna ambavyo ulimwengu unapima maisha ya ushindi hufanana kwa namna fulani ambavyo Wayahudi walipima ushindi. Lakini bado, wale waishio katika dhambi, nje ya Krsito, watashtukia wamekuwa watumwa wa dhambi, Yohana 8:34-36. Kwa kifupi, wale wanaousaka ushindi nje ya Kristo wanachofanya ni moja ya aina ya kujidanganya ambayo ulimwengu umepata kuona.

Unautaka ushindi? Ushindi unapatikana na uko katika Kristo pekee! Unataka mwishoni usimame ukiwa mshindi? Basi acha kujaribu kuupata ulimwengu wote, Marko 8:36-37. Na kumbuka kuwa nje ya Kristo, tunakuwa ndani ya dhambi, Warumi 6:23. Ingawaje tunaweza kujipumbaza wenyewe kwa kuamini kuwa mwishoni tutasimama washindi bila Yeye. Bila damu yake kuwa upande wetu, hatuna matumaini, Warumi 5:9. Tukiwa na damu yake upande wetu tuliyogusana nayo katika ubatizo (Warumi 6:1-4; Mdo 22:16; Waebraania 9:22) huku tukiwa tunadumu ndani yake kwa kuishi maisha ya uaminifu (1Yohana 1:7-9; Ufun.2:10). Lakini Mungu na ashukuriwe atupaye kushinda kwa Bwana wetu Yesu Kristo”, 1 Wakorintho 15:57.